

ISHARA YA MASIHI



Hebu tuinamishe vichwa vyetu kwa dakika moja.

Mungu mpendwa, tunapousikia wimbo huo, “Yesu yu karibu, na mambo yote yanawezekana,” inaisisimua mioyo yetu kujua kwamba huo ni zaidi ya wimbo. Ni Ukweli. Uko hapa. Bwana, naamini ulikuwa tu nyuma ya maskani sasa hivi, pia; maskini yule mama akiwa amemshika mtoto huyo mchanga, amelowa kabisa, kwenye mvua; na huyo kijana mwanamume akimwita mpendwa wake, huko mbali hospitalini, akifa. Yasikie maombi yetu, Bwana. Kuna watu wameketi katika kanisa hili siku nzima, tangu saa thenashara asubuhi ya leo. Wanangojea kukuona Wewe, Bwana. Wametusia tukizungumza leo kwamba ulifufuka katika wafu. Nawe ni Yesu yeye yule ungali unaishi usiku wa leo, baada ya miaka elfu moja na mia tisa. Ungali ni Yesu. Nasi tunaomba, Mungu, ya kwamba Wewe utamponya kila mgonjwa aliye katika Uwepo wa Kiungu. Jalia kusiwe na mtu mnyonge katikati yetu wakati ibada hii itakapomalizika. Tuonyeshe tu, Bwana, ya kwamba Wewe uko hapa.

² Tunawazia juu ya watu wawili katika asubuhi ile ya Pasaka, waliokuwa wamevunjika moyo. Hapana shaka, lakini wengi hapa wamevunjika moyo usiku wa leo, wagonjwa wala hawawezi kupona, madaktari wamewakatia tamaa. Nao walipokuwa wakienda zao, palikuwako na Mgeni aliyejitokeza na kuzungumza nao, akazungumza juu ya Maandiko, siku nzima. Na wakati wa usiku, alipowaingiza chumbani na kufunga mlango, Yeye alifanya jambo fulani. Alilifanya jinsi tu alivyolifanya kabla ya kusulubiwa, nao wakajua ya kwamba huyo alikuwa ni Bwana aliyefufuka. Alitoweka mbele ya macho yao. Wakakimbia haraka, wakarudi wakawaambie wengine, “Amefufuka katika wafu.”

³ Mungu, tunaomba ya kwamba atakuja katikati yetu usiku wa leo na kufanya mambo ambayo alifanya kabla ya kusulubiwa Kwake. Miaka elfu moja mia tisa si kitu Kwake; Yeye ni wa Milele. Basi jalia wengi hapa usiku wa leo wakimbie nyumbani haraka, wakiwaambia wake zao, mume wao, wapendwa wao, jirani yao, “Yu hai! Alinitokea usiku wa leo! Aliyaponya maradhi yangu! Nitakuwa mzima sasa.” Lijalie hili, Baba. Tunaomba katika Jina la Yesu. Amina. (Mwaweza kuketi.)

⁴ Samahani kwamba nimepwelewa na sauti, lakini nimekuwa tu na shughuli nyingi sana nikizungumza, nikibatiza; nilikuwa na mafua, kwanza kabisa, tangu niliporudi kutoka huko chini Florida na kule visiwani. Inabidi niondoke asubuhi sasa, kuelekea California, kwa karibu mwezi mzima wa mikutano.

Kwa hiyo nilimwomba Ndugu Neville kama angezungumza kwa niaba yangu usiku wa leo, nami nina hakika mmesikia ujumbe mzuri sana. Tulifurahia ibada ya asubuhi ya leo kutoka kwa Ndugu Neville. Nasi tunatumaini kwamba Mungu ataendelea kuwa pamoja naye na kanisa hili, anapofanya uchungaji hapa.

⁵ Sasa nimekutana na Billy hivi punde huko nje, naye kidogo akanigusa ubavuni, na akasema, “Baba, watu wamesimama hapa, na baadhi yao wamekuwa hapa siku nzima.”

⁶ Nikasema, “Vema, nina furaha kwamba ibada zetu zinaelekea kwisha, kwa hivyo haitawabidi kusimama.” Nayo mvua inanyesha. Na wakati nilipoingia humu jengoni, maskini mume na mke fulani walikuwa wakitoka kwenye gari huko nje, wakiwa na mtoto mchanga mgonjwa, naye alikuwa amelowa maji. Hangeweza hata kuingia milangoni. Lakini kwa hakika kama ninavyosimama hapa, Mungu alimponya mtoto huyo mchanga, tukiwa tumesimama pale nje. Um-hum. Jinsi Yeye anavyojibu maombi!

⁷ Na sasa baada ya sisi kuhubiri leo, na asubuhi ya leo nimehubiri juu ya masomo matano: *Kuishi, Kufa, Kuzikwa, Kufufuka, Kuja*.

Maishani, alinipenda; kifoni, akaniokoa;
Alipozikwa, alipeleka dhambi zangu mbali
kabisa;
Alipofufuka, alinihesabia haki bure milele:
Siku moja Yeye yuaja—loo, siku tukufu!

Tunaketi, tukikesha usiku wa leo, tukikungojea kuonekana Kwake.

⁸ Ni kwa nini tumesongamana humu ndani? Ni kwa nini watu huja kuisikia Injili? Hata hivyo, katika urahisi Wake, Ndiyo kivutio kikuu zaidi ulimwengu umewahi kuwa nacho. Yesu alisema, “Nikiinuliwa juu, nitawavuta watu wote Kwangu.” Sasa jambo ni kwamba, je, hii dini tunayoizungumzia, ni ya kweli? Ni Kweli? Kama ni Kweli, basi tunaweza kuamini kila Neno Biblia ililosema. Kama si Kweli, hatupaswi kuwa na uhusiano wowote nayo, tunapaswa kuendelea tu katika dhambi zetu; tule, tunywe, maana kesho tutakufa. Lakini ninashukuru sana kujua ya kwamba Hii tunayozungumzia ni ya Kweli! Na ndiyo dini pekee ulimwenguni... Walakini, ya nne kwa wingi, hata hivyo ndiyo dini pekee ulimwenguni ambayo Mwanzilishi wake angeweza kufa na kufufuka tena, na yu hai usiku wa leo.

⁹ Niliona kwenye gazeti, hapa kwenye gazeti la mji hivi majuzi, ambapo wana mtu, Mbuddha, aliyekuwa ameinuliwa. Wengi wenu waliona hilo kwenye gazeti. Wana mtu ambaye ni maskini Mbuddha anayefanya mambo kama tu Buddha alivyofanya; bila shaka, hakufanya miujiza yoyote, lakini mafundisho yake na kila kitu kilikuwa tu kama Buddha.

Kama Buddha ana mtu uwanjani, wa uongo; Mungu ana Roho Mtakatifu uwanjani, Roho halisi wa Mungu.

¹⁰ Sasa, tulizungumza juu ya mambo haya ya ajabu, lakini je, yatafanya kazi? Je, Mtakatifu... Je, Roho Mtakatifu atamsamehe mtu dhambi zake? Je, atamponya maradhi yake? Hakika atamponya. Yeye ni Mungu, hata milele. Sasa, kama tunaweza... Kama Yesu atakuja katikati yetu na atajithibitisha Mwenyewe, ya kwamba yu hai, hapa usiku wa leo miongoni mwetu, inapaswa kumfanya kila mmoja wetu kuamini kila ahadi Yeye aliyo nayo katika Biblia.

¹¹ Je, kuna mtu yeyote hapa ambaye hajawahi kuwa katika mojawapo ya mikutano yangu hapo awali? Hebu tuone mikono yenu, hujawahi kuwa mkutanoni hapo awali. Angalieni tu, karibu nusu ya umati!

¹² Mimi si mponyaji. Siamini—siamini kuna mtu ambaye ni mponyaji. Yesu Kristo ndiye Mponyaji.

¹³ Naye alisema, alipokuwa hapa duniani, ya kwamba Mungu ndiye Mponyaji. Sasa, alipokuwa hapa duniani, hakudai kuwa Mponyaji, bali aliwaonyesha watu ishara Yake ya Kimasihi, nayo ishara hiyo ya Kimasihi ilikuwa ni kujua siri za moyo wao. Ni wangapi wanaojua hiyo ni kweli?

¹⁴ Wakati alipomwambia Petro, alipokuja mbele Zake, jina lake lilikuwa nani, jina la baba yake lilikuwa nani; Petro aliamini sana kwa njia hiyo, na imani kubwa mno, hivi kwamba Yesu alimpa funguo za Ufalme, baadaye, na kumweka juu ya Kanisa.

¹⁵ Filipo alipomkuta Nathanaeli chini ya mti, na kumwambia, “Njoo uone niliyemwona, Yesu wa Nazareti, mwana wa Yusufu.”

¹⁶ Naye huyo mwanadini shupavu akasema, “Laweza neno lolote jema kutoka Nazareti?”

¹⁷ Alimpa jibu zuri sana ambalo mtu yeyote angeweza kutoa. Alisema, “Njoo uone. Usilikosoe tu. Njoo, ujionee mwenyewe.”

¹⁸ Na mara Filipo alipokuja pamoja na Nathanaeli, Yesu alimwambia, “Tazama Mwisraeli kwelikweli ambaye hamna hila ndani yake!”

Akasema, “Ulinijua lini, Rabi?”

Akasema, “Kabla Filipo hajakuita, nilikuona chini ya mti.”

Akasema, “Wewe ni Mwana wa Mungu, Mfalme wa Israeli.”

¹⁹ Alimwambia yule mwanamke kisimani yale yaliyokuwa moyoni mwake. Mambo haya yalithibitisha ya kwamba Yeye alikuwa ndiye Masihi. Na kama Masihi huyo amefufuka katika wafu leo, na amefanya upatanisho, na kuyaponya maradhi yetu na kutusamehe dhambi zetu, basi jambo pekee angeweza kufanya lilikuwa ni kuonyesha ishara iyo hiyo tena, kwamba Yeye yungali hai apate kutimiza ahadi yoyote aliyofanya. Hiyo ni kweli? Hebu na tuamini hilo sasa tunapoomba.

²⁰ Bwana, watu wanangoja. Neno moja kutoka Kwako litakuwa ni zaidi ya yale mimi ama Ndugu Neville tungeweza kusema katika muda wa maisha mengi. Neno moja tu. Sasa, kuna nusu ya wasikilizaji hawa ambao hawajawahi kuona hii mikutano hapo awali. Bwana Mungu, Muumba wa Mbingu na nchi, tuma Nguvu za Yesu Kristo kwenye chumba hiki, Yeye aliyefufuka, yule Roho Mtakatifu aliyekuja kwenye Pentekoste, na jalia awatie watu mafuta sana. Jalia niweze, hata katika kupwelewa huku na sauti, kujitoa kikamilifu sana kwa Roho Wake, ili aweze kunena kupitia sauti hii iliyopwelea ninayomtolea, aangalie kupitia macho haya ninayomtolea Yeye, kuonyesha maono na mambo ambayo yangewafanya watu kuona ya kwamba amefufuka katika wafu. Ndipo watu hawa watakapoona hilo, jalia kusanyiko zima liikumbatie kila ahadi aliyotoa. Ikiwa wametenda dhambi, jalia wamkumbatie kwa ajili ya msamaha. Kama wana ugonjwa, jalia wajue kwamba kwa kupigwa Kwake sisi tumeponywa. Tujalie, Bwana. Tunaomba katika Jina la Yesu. Amina.

²¹ Sasa hili hapa shindano kubwa la kuamua. Hapa, mbele ya watu mia mbili au mia tatu, ni rahisi. Unaposimama mbele ya laki tano, nusu milioni, mambo yale yale yanatukia. Yeye ni Mungu. Sasa ni wangapi humu ndani walio wagonjwa na wanataka kuombewa, inueni mikono yenu. Mnaona, karibu nusu yenu, au zaidi. Siwezi kuwaleta wote hapa. Nafikiri... Itanibidi kumwuliza Billy tena. (Mwulize kama alisambaza kadi za maombi. Sasa, alifanya hivyo—alizisambaza?) [Mtu fulani anasema, “Ndiyo.”—Mh.] Vema. Vema.

²² Jumapili iliyopita au mara ya mwisho nilipokuwa hapa, hawakusambaza kadi zozote za maombi, nami nikauliza tu, “Ni watu wangapi hapa hawajawahi kuwa kwenye mkutano hapo awali?” Wengi wakainua mikono yao, ya kwamba hawakuwahi kuwa mkutanoni. Wakiwa wamesimama huku wameinua mikono yao, Roho Mtakatifu akaendelea, akiwaambia wao ni nani na magonjwa yao yalikuwa nini, na yale yaliyokuwa yametukia; na kuwaponya watu kikamilifu sana, mpaka vivimbe na kadhalika vikatoweka, hata upasuaji haukuweza kufanywa. Ni wangapi walikuwa hapa kuona hilo majuma machache tu yaliyopita?

²³ Kama amesambaza kadi za maombi, basi tutawaita. Hiyo huwapa watu wa nyumbani, na watu wasio wa nyumbani; watu ambao wamekuwa mkutanoni, watu ambao hawajawa mkutanoni; kuja katika mstari wa maombi. Hatuwezi kuwaleta wote hapa mara moja. Tutawaleta kimya kimya tu kadri tuwezavyo.

²⁴ Nami nataka uwe mwaminifu kwa Mungu. Uwe mwaminifu kwa nafsi yako mwenyewe. Na ikiwa Yesu Kristo atakuja katikati yetu na kufanya na kutekeleza kama vile tu alivyofanya alipokuwa hapa duniani, akitembea huko Galilaya, unapaswa

kumkubali kwa chochote unachohitaji. Si lazima uwe hapa jukwaani. Anaijali imani. Kutakuwa na baadhi ya watu hapa ambao ni wagonjwa huko nje kwenye kusanyiko, ambao hata hawana kadi ya maombi, wataponywa kwa vyovyote vile. Ni wangapi walio wagonjwa wala hawana kadi ya maombi? Inueni mikono yenu. Vema, hakuna kadi nyingi sana za maombi zilizosambazwa basi, mnaona. Vema, wewe amini tu. Angalia tu huku.

²⁵ Hebu niwaonyeshe yale Yesu aliyofanya alipokuwa hapa duniani. Kulikuwako na mwanamke, wakati mmoja, aliyemjia. Wala asingeweza kuingia kwenye huo umati. Hakuwa na kadi ya maombi, bali aligusa upindo wa vazi Lake, kwa maana alisema moyoni mwake, “Ninajua Mtu yule husema Kweli. Kama ninaweza kugusa vazi Lake, nitapona.” Naye akaligusa vazi Lake, akaingia kwenye kusanyiko labda kubwa mara nyingi zaidi ya hili.

Yesu akageuka, na kusema, “Ni nani aliyenigusa?”

²⁶ Hata Petro akamkemea, akasema, “Kwa nini uulize kitu kama hicho, wakati wote wanajaribu kukugusa?”

Akasema, “Lakini naona nimekuwa dhaifu.”

²⁷ Maono husababisha udhaifu. Huwezi kufanya, kwenda mbali sana katika hayo. Naye akasema, akatazama huku na huku juu ya kusanyiko mpaka akampata yule mwanamke, na kumwambia kwamba alikuwa anatokwa na damu, na imani yake ilikuwa imemponya.

²⁸ Ni wangapi wanaojua hilo? Biblia ilisema kwamba, “Yesu Kristo leo ni Kuhani Mkuu anayeweza kuguswa na mambo ya udhaifu wetu.” Hiyo ni kweli? Vema, kama Yeye alikuwa ndiye Kuhani Mkuu, ambaye angeweza kuguswa na mambo ya udhaifu wetu, si angetenda tu kama vile alivyofanya wakati huo, endapo ni Yeye yule jana, leo, na hata milele?

²⁹ Basi wewe usiye na kadi ya maombi, angalia huku, na useme moyoni mwako, “Bwana, ninaamini kwa moyo wangu wote, nami ninaamini ya kwamba utaniponya. Basi nijalie niliguse vazi Lako. Nawe unene kupitia Ndugu Branham na kumwambia, kama vile tu ulivyomfanyia yule mwanamke, nami nitakuamini.” Je, utakuwa mwaminifu hivyo, na kumwamini Mungu kwa moyo wako wote?

³⁰ Billy Paul alisema, alisema dakika chache zilizopita, akisimama hapa, mlichukua sadaka ya upendo kwa ajili yangu. Sikutaka hili lifanyike. Hiyo ilikuwa . . . Lakini, asanteni, lakini. Ninaihitaji sasa kwenye safari yangu ya California. Nitaiweka kwenye Injili.

³¹ Hayo matoleo madogo mnayonipa, mnajua yanavyotumika? Nilienda Puerto Rico na Jamaica majuma machache yaliyopita, ambako waliandikisha waongofu elfu arobaini katika usiku tisa.

Ni kitu gani kilichosababisha hilo? Zaka zenu. Nilipoondoka, meya wa . . .hakimu wa kisiwani alisimama, akasema, “Tunao wainjilisti wanaokuja hapa na kuchukua matoleo makubwa, na inagharimu pesa nyingi. Lakini,” kasema, “Ndugu Branham alipokuja, hakuomba hata senti moja ya pesa, kamwe hakutuomba tulipe bili yake ya hoteli. Naye alilipa nauli yake mwenyewe, kwenda na kurudi.” Ni kitu gani kilichofanya hilo? Pesa zenu. Ninataka kuhakikisha kwamba ninaitumia vizuri. Ili kwamba, kwenye Kiti cha Hukumu, nitakaposimama mbele yenu na Mungu, inibidi kutoa hesabu yake, imefanywa ipasavyo. Niliichukua mwenyewe, maadamu ninaweza kwenda, kufanya vizuri niwezavyo kwa ajili ya utukufu Wake.

³² Sasa hatuwezi kuleta kadi zote za maombi huku juu mara moja, kwa hiyo nitawapandisha tu, wachache tu kwa wakati mmoja.

³³ Ni nani aliye na kadi ya maombi namba moja? Tafadhali inua mkono wako kama unaweza kusimama. Huko nyuma kabisa, ni mwanamke mweusi. Shuka moja kwa moja huku, mama. Shuka uje hapa kando ya jukwaa. Sasa ni nani aliye na kadi ya maombi namba mbili? Kama unaweza kusimama, inua mkono wako, kadi ya maombi namba mbili. Mwanamke mzungu hapa. Vema, mama, njoo papa hapa juu umfuate huyu mama mweusi hapa, papa hapa juu. Sasa wapisheni *hivyo*, Doc, mara huu utakapojaa hapa juu.

³⁴ Kadi ya maombi, namba tatu, naomba uinue mkono wako kama unaweza. Hao waungwana papa hapa, bwana. Namba nne, naomba uinue mkono wako. Vema, mama, papa hapa. Namba tano, naomba uinue mkono wako. Jamaa huyu mdogo hapa hapa. Kufikia sasa, kila mmoja wao ni wageni kwangu. Namba sita, naomba uinue mkono wako, namba sita. Je, niliita namba tano, namba tano? Na namba sita, pia mgeni kwangu. Namba saba, unaweza kuinua mkono wako? Inua mkono wako, uliye na namba saba. Vema, ninaamini ninamjua jamaa huyo. Na—naamini namfahamu. Namba nane, naomba uinue mkono wako kama unaweza. Mama mmoja hapa. Vema, nambari tisa. Vema, mama. Namba kumi. Vema, namba kumi, yule mama.

³⁵ Kuna kosa mahali fulani. Huyu mtu hapa ni namba ngapi? Naomba mtu fulani aangalie, baadhi yenu mabawabu njoni hapa muone. [Mtu mmoja anasema, “Yeye ni themanini na nne.”—Mh.] Themanini na nne. Nilikuwa nikiita namba kumi basi, asante, namba kumi. Lakini tutakufikia kwa vyovyote vile. Hiyo ni sawa. Angalia, najua namba yako ni ipi sasa. Ni themanini na nne, siyvo, unasema themanini na nne ama kitu kama hicho? Vema, ngojea tu hapo. Wewe amini tu. Ninakwambia, kama hutumii kadi hiyo, kadi ya maombi, angalia huku na kumwamini Mungu, uone kama Mungu atakujibia maombi. Vema.

³⁶ Namba, hiyo ilikuwa kumi? Kumi na moja. Vema, kumi na

mbili. Sasa, kama huwezi kusimama, ninii tu. . . Namba kumi na mbili. Kumi na tatu, namba kumi na tatu, huko nyuma kabisa. Kumi na nne, namba kumi na nne, huko nyuma kabisa. Namba kumi na tano.

³⁷ Zinasambazwa popote. Wavulana wanaozisambaza, wanasema tu, “Ni nani anayetaka kadi ya maombi? Inueni mikono yenu.” Wanazichukua na kuzichanganya zote, hakuna ajuaye ni yupi anayepata ipi. Na wanazisambaza hivyo tu.

³⁸ Namba kumi na nne. Namba kumi na tano, ni nani aliye na kadi ya maombi kumi na tano, namba kumi na tano? Namba kumi na sita, huko nyuma kabisa. Namba kumi na saba. Sasa, kama namba kumi na sita yuko humu jengoni au amesimama kwenye marefu ya kanisa, jongea tu huku. Namba. . . Samahani, kamwe sikuuona mkono wako, dada, juu yake. Wewe ni kumi na sita? Vema. . . [Dada huyo anasema, “Kumi na saba.”—Mh.] Kumi na saba. Kumi na nane, kumi na tisa, namba kumi na tisa. Ishirini, namba ishirini, huyu mtu hapa. Vema. Vema.

³⁹ Sasa naamini tunaingia moja kwa moja kwenye marefu ya kanisa sasa, kwa hiyo tutaninii. . . [Ndugu fulani anasema, “Hao wametosha.”—Mh.] Wasemaje? [“Hao wametosha.”] Hao wametosha kwa wakati huu. Sawa. Vema, angalieni huku na muamini. Vema.

Hebu tuone, kama mpiga piano, kwa upole na utulivu, *Amini Tu*, polepole kabisa.

⁴⁰ Karibu watu wote kwenye marefu ya kanisa hapa hatufahamiani. Siwajui ninyi. Sasa kuna wengine humu ndani ambao bado wana kadi za maombi, wengine labda hawana kadi za maombi. Labda tunaweza kuwaita wengine zaidi katika mstari wa maombi katika dakika chache tu, mara tutakapomalizana na marefu haya ya kanisa.

⁴¹ Ninaamini muungwana huyo hapa, Doc, alikuwa akiingia kutoka nyuma kule, aliitwa, kumi na sita ama saba- . . . kumi na sita. Vema, njoo moja kwa moja hapo uchukue mahali pako, bwana.

⁴² Sasa, kama hujaitwa, hilo halina uhusiano wowote nalo, unaona, angalia tu na uamini.

⁴³ [Ndugu fulani anasema, “Kumi na tano ingali imekosekana, pia.”—Mh.] Nambari kumi na tano haipo. Labda huyo mtu hawezi kusimama. Ikiwa huwezi kusimama. . . Mtu fulani aangalie kadi ya maombi ya mtu mwingine, labda yeye ni kiziwi na hawezi kusikia. Ikiwa wako hapa, kumi na tano, umekaribishwa kuchukua nafasi yako mstarini. Ikiwa walitoka nje na watarudi katika dakika chache, waweke mstarini wakati tu namba yao inapoitwa.

44 Tukishuka mstarini hapa, tutaita wengine zaidi, kama Roho Mtakatifu haonekani kutia jengo mafuta, hao watu, wapate kuponywa.

45 Sasa, sasa ni wakati muhimu, sasa ndio wakati ambapo ama nimesema Kweli au nimesema uwongo. Sasa ndio wakati ambapo Yesu Kristo anathibitishwa kuwa amefufuka katika wafu, au hajafufuka katika wafu. Sasa ndiyo wakati Yeye ni yeye yule jana, leo, na hata milele, ama Yeye si yule yule jana, leo, na hata milele. Sasa hana budi kuthibitisha kuwa ni Mponyaji, ama Yeye si Mponyaji. Na kama mtu yeyote angetaka kupachukua mahali pangu, kuwaombea wagonjwa, umekaribishwa uje upachukue mahali pangu.

46 Ni wangapi wenu katika mstari wa maombi hapa, mnapotazama hapa, walio kwenye mstari wa maombi sasa, hawanijui, nawe unajua sikujui wewe wala chochote kukuhusu, inueni mikono yenu.

47 Huko kwenye kusanyiko, ambaye unajua kwamba sijui chochote kukuhusu, inua mkono wako (hata hivyo u mgonjwa) huko kwenye kusanyiko. Mnaona, haya basi.

48 Sasa Mungu atafanya nini? Hayo hapo Maandiko, Roho wa Mungu yuko hapa, sasa je, itafanya kazi? Nikiweza kujitolea kwa Roho Mtakatifu, itafanya kazi. Wala haitafanya kazi kwangu isipokuwa ujisalimishe kwa Roho Mtakatifu, “Kwa maana miujiza mingi Yesu hangeweza kufanya katika nchi Yake Mwenyewe, kwa sababu ya kutokuamini kwao.”

49 Sasa amini kwa moyo wako wote, iweni na kicho sana mwezavyo. Simameni kimya, angalieni. Kama Roho Mtakatifu akifanya jambo, basi furahini, kisha muamini.

50 Sasa, Bwana, yote tuliyo nayo, yote tuliyo. . . Wamesimama mpaka miguu yao inakakamaa, wamekaa mpaka nusura wazimie. Sasa, Bwana, na ijulikane ya kwamba Wewe ni Mungu. Nami nimeliita kusanyiko hili pamoja, kwa amri Yako. Nami nimesimama hapa, sio nipate kuonekana, ama sio kujifanya mkubwa au kufanya jambo tofauti, bali ni kwa sababu ni agizo nililoagizwa na Malaika, na kuthibitishwa na Neno Lako. Na ijulikane usiku wa leo ya kwamba Wewe ni Yesu Kristo, Mwana wa Mungu, aliyefufuka katika wafu; Nawe unaishi katika Kanisa Lako, ndani ya watu Wako, kufanya na kutekeleza huduma ile ile uliyokuwa nayo ulipokuwa hapa katika mwili wa nyama. Tujalie, Bwana. Nasi tutakutukuza Wewe, katika Jina la Yesu Kristo. Amina.

51 Sasa Billy Paul yuko wapi, yuko humu jengoni? Je, ameondoka? Ama, mtu fulani anapaswa kuja hapa kuchukua hizi kadi za maombi, unaona. Njoo, Ndugu...?...Huyu mwanamke ana kadi ya maombi mkononi mwake. Wewe mpe tu, unaona.

Iweni na kicho kabisa sasa.

⁵² Sasa mama huyu hapa, nijuavyo mimi, ni mgeni kabisa kwangu. Basi haya hapa mandhari makamilifu ya Maandiko, watu wawili na mataifa mawili mbalimbali.

⁵³ Yesu alikuja kwenye kisima wakati mmoja, katika Yohana Mtakatifu 4, akakutana na mwanamke Msamaria. Ndipo akazungumza naye kwa muda kidogo, mpaka akapata kujua shida yake ilikuwa ni nini. Naye akamwambia shida yake. Ndipo, alipofanya hivyo, akatambua kuwa ni Masihi. Ni wangapi wanaojua jambo hilo? Mnakumbuka mazungumzo yao? Alisema, “Mwanamke, nipe maji ninywe.” Yeye alikuwa akifanya nini? Akiwasiliana na roho yake.

⁵⁴ Naye akasema, “Kisima ni kirefu, Nawe huna kitu cha kuchotea. Sio kawaida Kwako, Myahudi, kuwaomba Wasamaria kitu kama hicho.”

⁵⁵ Akasema, “Lakini kama ungalijua ni nani uliyekuwa ukizungumza naye, ungeniomba Mimi maji.”

⁵⁶ Na kwa hiyo mazungumzo yakaendelea mpaka Yeye akagundua shida yake ilikuwa nini. Ni wangapi wanajua shida yake ilikuwa nini? Alikuwa akiishi katika uzinzi. Kwa hiyo akasema, “Nenda kamwite mumeo uje naye hapa.”

Akasema, “Sina mume yeyote.”

⁵⁷ Kasema, “Hiyo ni kweli. Umekuwa na watano, na yule unayeishi naye sasa siye mume wako.”

⁵⁸ Sasa sikilizeni alichosema. Akasema, “Bwana, naona ya kuwa Wewe ni Nabii. Tunajua Masihi atakapokuja Yeye atatwambia mambo haya. Yule Masihi, ishara ya Masihi, Yeye atafanya hivi atakapokuja; maana Yeye alikuwa ni Mungu-Nabii, Nabii, Musa alinena habari zake.” Kasema, “Tunajua Masihi atafanya haya atakapokuja, lakini u Nani Wewe?”

Akasema, “Mimi ninayesema nawe Ndiye.”

⁵⁹ Ndipo akakimbilia mjini na kuwaambia hao watu, “Njoni, mwone Mtu aliyeniambia mambo niliyofanya. Haimkini huyu kuwa ndiye Masihi?”

⁶⁰ Basi huyu hapa amesimama mwanamke Mwethiopia pamoja na mwanamume Mwango-Sakson, mara ya kwanza kukutana maishani; tunaowaita mwanamke mweusi, mwanamume mzungu. Swali hilo lilipoulizwa pale, katika ule ubaguzi, mbele ya Yesu, Yeye aliwafahamisha upesi sana: hakuna tofauti katika rangi za watu. Sisi sote tunatoka kwenye mti mmoja, Adamu na Hawa. Kweli kabisa. Nchi tulizoishi, zilibadilisha rangi yetu; haikuwa na uhusiano wowote nayo. Mungu alikufa kwa ajili ya viumbe vyote: mzungu, mtu mweusi, mtu wa manjano, mtu wa kahawia, mtu mwekundu, na wote. Wote ni viumbe vya Mungu.

⁶¹ Lakini huyu mama amesimama hapa kwa ajili ya jambo fulani. Labda yeye ni mwaminio, labda siye. Labda yeye ni mwenye dhambi. Huenda akawa ni mtakatifu. Huenda akawa ni

mgonjwa, huenda asiwe. Huenda akataka; matatizo ya kifedha. Huenda ikawa amesimama kwa niaba ya mtu mwingine. Sijui. Sijawahi kumwona, wala sina fununu kamwe ya kilichomleta hapa. Naye huyu mama anajua hilo. Hiyo ni kweli, mama? [Dada huyo anasema, “Ndiyo, bwana.”—Mh.] Kama hiyo ni kweli, inua mkono wako ili watu waweze kuona. Inua tu mkono wako kusudi watu. . . Inua tu mkono wako. Hii ndiyo mara yetu ya kwanza kukutana. Sasa kama Bwana Yesu ataninii. . .

⁶² Kama yeye ni mgonjwa, nisingeweza kumponya zaidi ya vile nisingeweza kukuponya. Lakini ikiwa—ikiwa Yesu yuko hapa asingeweza kumponya, kwa maana Yeye tayari alimponya alipokufa pale Kalvari. Lakini Yeye anaweza kufanya jambo fulani kuthibitisha ya kwamba Yeye angali ni Yesu yeye yule, naye angeamini, angeponywa. Na wakati ule ule yeye angeponywa, wewe ungeponywa, pia, kama ungeamini hilo. Je, hiyo ni kweli? Sasa, Bwana na atujalie. Ninangojea upako wa Roho Mtakatifu, bila shaka.

⁶³ Na sasa, katika Jina la Yesu Kristo, ninachukua kila roho humu ndani chini ya mamlaka yangu, kwa ajili ya utukufu wa Mungu.

⁶⁴ Sasa, mama, nataka tu uniangalie kwa muda kidogo. Nakutaka uamini kwa moyo wako wote. Wala sina fununu ya kilichokuleta hapa, kwamba u nani wewe, hata kidogo. Lakini Mungu anajua yote kukuhusu. Lakini kama Mungu ataniambia kilichokuleta hapa, basi utaamini kwamba Yesu Kristo, Mwana wa Mungu, yuko hapa kufanya na kutenda jinsi Yeye alivyofanya alipokuwa hapa duniani?

⁶⁵ Je, kusanyiko litaamini, kwa nia moja?

⁶⁶ Sasa sisi hapa, mandhari yamewekwa. Sote wawili tumeinua mikono yetu juu, hatufahamiani. Roho Mtakatifu aliandika Biblia, akasema mambo haya yangetukia katika siku hii, kwamba Yesu alikuwa amefufuka katika wafu na mambo haya yangeendelea, huduma Yake ingeendelea, na katika siku hizi za mwisho ingekuwa vile vile tu kama alivyoahidi itakuwa. Sasa je, ni kweli?

⁶⁷ Mama huyo, kwa vile ana wasiwasi, bila shaka, anasugua mikono yake kwa sababu anajisikia kigeni wakati huu. Si kwa sababu amesimama karibu nami; mimi ni ndugu yake, isingemfanya kujisikia hivyo. Lakini yeye ni—anafahamu kwamba jambo fulani linaendelea. Nawe unaona picha ile pale pamoja na hiyo Nuru juu yake, dada? Hiyo ndiyo inayokufanya ujisikia hivyo. Huyu ni yule Malaika wa Bwana, Yuko papa hapa juu yako sasa hivi. Nawe uko hapa nipate kukuombea, kwa tatizo la mgongo linalokusumbua. Hiyo ni kweli, inua mkono wako.

⁶⁸ Sasa unaamini? Unaona, kufanya ijulikane, siri ya moyo. Kama tu vile Yeye alivyosema, “Una waume watano.”

⁶⁹ Unasema mimi...sasa, wageni, huenda mkasema, “Ndugu Branham alibahatisha jambo hilo.”

⁷⁰ Hebu tuone kama ilibahatisha. Ninaamini ilisema ulikuwa na tatizo la mgongo. Hiyo ilikuwa kweli? [Dada huyo anasema, “Ndiyo.”—Mh.] Huo ulikuwa ni ukweli? [“Ndiyo, bwana.”] Nawe, umefanyiwa upasuaji, pia, na umetoka hospitalini hivi punde tu. Na, ili upate kujua ya kwamba mimi ni mtumishi wa Mungu, mumeo ameketi pale nyuma. Naye ana tatizo, pia. Nikiweza kukwambia tatizo la mumeo ni gani, utaamini? [“Naam, bwana.”] Ana tatizo la ubavu wake na mgongo wake. Hiyo ni kweli? Inua mkono wako. Nitakwambia jambo lingine. Ninamwona kijana mwanamume, mwanao, ameketi moja kwa moja pale nyuma, pia. Kweli. Naye mwanao ana aina fulani ya kifafa. Hiyo ni kweli. Bibi Stovall ndilo jina lako. Hilo ndilo jina lako, Bibi Stovall. Nenda nyumbani, Yesu Kristo amejibu maombi yako! Unaweza kupata ulichomba, katika Jina la Yesu.

⁷¹ Sasa aminini tu! Ninyi watu wote ambao ni watu weusi, amini kwa moyo wako wote sasa. Je, unatambua kwamba Yesu Kristo, Mwana wa Mungu, amefufuka katika wafu? Huyu ni Roho Wake anayekufanya ujisikie hivyo.

⁷² Sasa huyu hapa mwanamke mzungu. Simjui, sina fununu yeye ni nani, kile alichokuleta hapa. Kama hiyo ni kweli, inua mkono wako. Sasa unaamini? Kama Mungu akipenda, akiweza kuufunua moyo wake, kama tu alivyomfanyia yule mwanamke kisimani, kama alivyomfanyia yule mwanamke mweusi, ni wazungu wangapi wangeamini kama angefanya hivyo? Hapa, mimi na mwanamke huyu, sote wawili tukiwa tumeinua mikono yetu, hii ndiyo mara yetu ya kwanza kukutana.

⁷³ Ninasema jambo moja, mama huyo hatoki karibu na hapa. Umetoka mashariki, ulikuja magharibi ulipokuja hapa. Hiyo ni kweli. Umetoka Ohio, nao huo mji ulikuwa Dayton. Hiyo ni kweli. Na kilichokuleta hapa, ni kwa sababu una udhaifu. Pia una ugonjwa wa fadhaa, kwa sababu huwezi kulala. Unakunywa namna fulani ya dawa kwa ajili yake. Wanakuita “Dixie,” hiyo ni kweli, Mason. Hiyo ni kweli. Rudi, utalala sasa, tangu usiku wa leo na kuendelea. Yesu Kristo anakuponya. Nenda katika Jina la Bwana.

⁷⁴ Kama unaweza kuamini! Sasa ninyi huko nje katika wasikilizaji, wakati upako wa Roho Mtakatifu ukiwa hapa, aminini, ninyi msio na kadi za maombi.

⁷⁵ Vipi kuhusu yule mzee aliyesimama hapa muda mfupi uliopita, ambaye, hangeweza kuwa...asingeweza kuingia mstarini, alikuwa na namba nyingine, alikuwa wapi? Wewe, simama kwa miguu yako. Je, unamwamini Yesu Kristo kuwa ni Mwana wa Mungu? Je, unaniamini mimi kuwa ni nabii Wake? [Ndugu huyo anasema, “Naam, bwana.”—Mh.] Vema. Una

tatizo la mapafu yako. Hiyo ni kweli. Limekuacha sasa, nenda nyumbani na uwe mzima! Yesu alikuambia pafu zuri, unaona.

Iweni na imani, na mwamini. Mungu ni Mungu.

⁷⁶ U hali gani, bwana? Je, unamwamini Bwana Yesu Kristo? [Ndugu huyo anasema, “Amina.”—Mh.]

⁷⁷ Sasa, kulikuwa na mtu mmoja aliyemjia Yesu wakati mmoja, naye akaenda akaokoka, kisha akaenda akamwambia rafiki mwingine, akamleta. Basi huyu rafiki . . . Alimwambia kwamba ni mwaminio. Naye akastajabu aliposikia, ndipo akasema, “Ulipata kunijua lini?”

⁷⁸ Akasema, “Kabla Filipo hajakuita, ulipokuwa chini ya mti, nilikuona.” Hiyo ilikuwa maili thelathini kuzunguka mlima. Kwa miguu, ilimchukua siku nzima kurudi kwenye mstari wa maombi, na alipoingia kwenye mstari wa maombi.

⁷⁹ Je, unaamini kwamba Yesu anaweza kuniambia shida yako ni nini? [Ndugu huyo anasema, “Naam, bwana.”—Mh.] Je, ungeamini kwa moyo wako wote? [“Naam, bwana.”] Je, kusanyiko litaamini kwa moyo wao wote? Hayuko hapa kwa ajili ya nafsi yake. Ni kwa ajili ya mtu mwingine; na huyo ni mwanamke, naye ametiwa uvuli wa mauti, huyo ni dada yako. Sio nanii wako hasa . . . Ni dada yako wa kambo. Naye hayupo hapa. Yuko hospitalini huko Tennessee. Vivyo hivyo wewe umetoka huko. Na wewe ni . . . Huyo mwanamke alifanyiwa upasuaji, lakini haikusaidia chochote. Na wewe umesimama kwa niaba yake. Mungu akupe haja yako. Nenda zako, na Mungu amponye mwanamke huyo na kumpa afya, juu ya msingi wa imani ya mwanamume huyu.

⁸⁰ Bwana Mungu, tunamhukumu ibilisi huyo ambaye anauchukua uhai wa mwanamke huyo. Na jalia mtu huyu, ambaye ni jamaa yake, aishi kwa sababu amekuja na kusimama mahali pake. Yesu, Wewe ulisimama pale Kalvari badala yetu, Nawe ukatuponya. Nasi tunakuamini Wewe. Na iwe hivyo. Amina.

Nenda, ukiamini sasa, ndugu. Usiwazie lolote lingine.

⁸¹ U hali gani? Hatufahamiani. Hii ni mara yetu ya kwanza kukutana. (Sasa iweni na kicho sana, na msikilize kwa makini na mwombe.) Iwapo hatufahamiani, nasi ni wageni, mmoja kwa mwingine labda mara yetu ya kwanza tumepata kukutana. Hiyo ni kweli? Ikiwa hii ndiyo mara ya kwanza tumepata kukutana, inua mkono wako. Kama Mungu atanifunulia mimi shida yako ni nini, basi utaniamini kuwa mimi ni mtumishi Wake? [“Naam, naamini ndiyo ulivyo. Wewe ni mtumishi wa Kristo.”] Nitakuambia sasa. Hatujawahi kukutana hapo awali, lakini wewe ni Mkentaki. Hiyo ni kweli. Umetoka mahali paitwapo Somerset, Kentucky. Hiyo ni kweli kabisa. Mimi ninatoka Burkesville, Kentucky. Na unateseka na shida ambayo iko tu—tumboni, matumbo, sehemu ya chini. Ni vivimbe. Hiyo ni

kweli. Vema, Jewel ["Loo!"], rudi, Mungu akupe uponyaji wako. ["Loo!"]

⁸² Je, unamwamini Mwana wa Mungu, Yesu aliyefufuka? [Dada huyo anapiga kelele tena, "Loo!"—Mh.] Kama unaweza kupokea! Mnaweza kushangaa ni kwa nini mama huyo anashangilia. Ungeshangilia, pia, ["Loo!"] kama ungekuwa katika hali ya kufa. ["Jina Lake lisifiwe!"]

⁸³ Sikujui wewe. Lakini mimi si... Kama sijakosea, ninaamini ulibatizwa asubuhi ya leo, maana naona umefanya jambo zuri. Lakini, kukujua wewe, sikujui. Uliingia tu kwenye kidimbwi, na hiyo ilikuwa... aka—akabatizwa. Lakini unaamini Yesu anaweza kunifunulia shida zako? Je, hili kusanyiko linaamini hivyo kwa moyo wao wote? Naona mwanamke akitokea kati yangu na wewe. Umesimama hapa kwa ajili ya mwanamke fulani, naye huyo mwanamke ana umri mkubwa sana kuliko wako. Mbona, ni mama yako. Hayupo hapa. Anatoka Georgia. Naye ana wasiwasi sana. Jambo ni kwamba, ni badiliko la maisha, kukoma hedhi. Nawe umesimama kwa ajili ya mama yako. Hiyo ni kweli. Vema, atapita hayo, na kuwa mzima. Nenda, ukiamini sasa, yote yatakwisha. Mwambie awe na ujasiri mzuri.

⁸⁴ Mungu akubariki, kijana mwanamume. Amini. Amini kwa moyo wako wote. Kama unaweza kuamini! Omba.

⁸⁵ Nadhani mimi na wewe hatufahamiani. Mungu anakujua Naye ananijua mimi. Lakini je, Mungu angeweza kunifunulia tatizo lako? Na kama angenifunulia, ungemwamini?

⁸⁶ Ni watu wangapi hapa ndani wangeamini, na kusema, "Mungu, nitaamini kama utamwambia mtu huyo?"

⁸⁷ Hebu kidogo. Mama anayeketi papa hapa nyuma ya wasichana hawa hapa, akinitazama, anasumbuliwa na kuvimba kwa mishipa ya damu. Naye ameketi hapo, akimwombea mtu mwingine. Nayo roho yake imemgusa Kuhani Mkuu, naye anawasiliana na Mungu. Unamwombea rafiki yako, aliye na ugonjwa wa akili. Na wanaishi katika m—mji, mji mdogo, ni Corydon, Indiana. Hiyo ni kweli. Ikiwa unaweza kuamini, unaweza kupata ulichoomba. Amina.

⁸⁸ Umekuwa na mshtuko wa moyo; umekaribia mwisho wa safari yako. Hebu nikwambie moja ya shida zako, hata hivyo, kuvuta sigara. Ngoja kidogo, roho hiyo iliruka wakati huo. Hataki kufanya hivyo. Hiyo ndiyo inayosababisha shida yako. Hapa, ni kijana *huyu* anayeketi papa hapa, anataka kuachana na sigara, pia. Kama ataamini kwa moyo wake wote, tabia ya sigara itaondoka. Kama unaweza kuamini! Unaamini? Kama utaliamini na kulifanyia kazi, unaweza kupata ukombozi wako; *nawe* pia. Hutoki hapa. Unatoka mbali na hapa, pia. Rudi Owensboro sasa, ukimsifu Bwana. Mwamini Mungu.

⁸⁹ Ninakujua, lakini sijui una shida gani. Ikiwa Bwana atanifunulia shida yako ni nini, utamwamini? Basi shida yako ya

tumbo itakwisha. Vema. Nenda nyumbani ukashangilie, amini kwa moyo wako wote.

⁹⁰ Siamini ninakufahamu. Je, hatufahamiani? [Dada huyo anasema, “Ndiyo.”—Mh.] Je, unaamini kwamba yale mimi...? Nikikwambia ukweli, utajua ni ukweli au la. [“Ndiyo.”] Vema, shida yako ya moyo itakuacha. Nenda zako nyumbani ukawe mzima.

⁹¹ Sikujui wewe, lakini Mungu anakujua. Unaamini kama ngingekwambia shida yako ilikuwa nini, na ilipokuwa, ungepona? Katika mgongo wako. Nenda zako nyumbani sasa, itakuacha na utakuwa mzima.

⁹² Unafikiri Mungu angeweza kuponya uvimbe huo na kuufanya mzima, bila upasuaji? Unaamini? Inua mikono yako kama unaamini. Nenda zako nyumbani ukaupokee, katika Jina la Bwana Yesu. Amini.

⁹³ Ajabu hii, niliposema hivyo, ulikuwa na jambo lile lile. Uvimbe. Ulipata hisia ya kigeni niliposema hivyo, maana roho zote mbili ziliruka, wakati ule ule. Nenda zako, Yesu Kristo atakuponya. Amini.

⁹⁴ Wewe ni kijana mwanamume, kuwa na ugonjwa wa yabisi kavu, lakini unaamini Yesu atakuponya? Kama unaamini, ondoka uende, ukiamini, ukaponywe.

⁹⁵ Ni wangapi wanaoamini kwa moyo wako wote?

⁹⁶ Vipi kama sikusema neno lolote kwako, lakini nikakuambia Mungu alikuponya ulipopiga kona pale nawe ukashikwa na hisia hiyo ya ajabu, ungeniamini? Nenda zako nyumbani, uko mzima. Yesu Kristo anakuponya.

⁹⁷ Wewe ni msichana mdogo anayesumbuliwa na fadhaa. Unaamini ya kwamba Mungu ataponya hiyo fadhaa na kuiondoa kwako? Umekuwa ukijaribu kutafuta mahali pa kuanzia. Ni hii papa hapa. Nenda zako sasa, ukishangilia, ukifurahi. Imekwisha, kwako. Amini kwa moyo wako wote.

⁹⁸ Una ugonjwa wa fadhaa ambao umesababisha ugonjwa wa tumbo. Uliponywa uliposimama pale nyuma, bwana. Hiyo ndiyo sababu nilikuwa nikikungoja upite. Endelea, kula chakula chako cha jioni, uwe mzima.

⁹⁹ Shida ya wanawake, wasiwasi, kufadhaika. Hiyo ni kweli. Itakuacha sasa. Nenda zako nyumbani ukapone, katika Jina la Bwana Yesu. Amini tu.

¹⁰⁰ Una ugonjwa wa kike, hiyo ni kweli, unasababisha mtiririko. Ni ovari iliyozibika. Amini, Yesu Kristo atakuponya. Nenda nyumbani, na uamini kwa moyo wako wote.

¹⁰¹ Sasa, una ugonjwa mbaya, uko moyoni mwako, kizuizi. Je, unaamini ya kwamba Yesu Kristo anakuponya? [Dada huyo

anasema, “Ndiyo.”—Mh.] Kama unaamini, nenda katika Jina la Bwana, ukawe mzima. Mwamini Mungu.

¹⁰² Vema, ndugu, unaamini ya kwamba Yesu Kristo anakuponya, pia? Shuka tu mstarini, ukimsifu tu Bwana.

¹⁰³ Ni wangapi huko nje sasa wanaomwamini Bwana Yesu? Anajua kila...

¹⁰⁴ Bibi Nash, ninakujua, lakini siwezi kuizuia Nuru hiyo inayoning’inia juu yako. Ninakujua, lakini unamwombea mtu mwingine. Ni mtoto mdogo, mtoto mdogo, haishi hapa. Anaishi huko Tennessee. Pia, unamwombea daktari rafiki yako ambaye ana shida ya moyo. Naye mkewe amepata kiharusi kidogo hivi punde. Hiyo ni kweli. Amini, na unaweza kuwa mzima.

¹⁰⁵ Msichana anayeketi mwishoni mwa kiti pale, ameweka kidole chake juu ya kinywa chake, unawazia nini, ewe msichana? Umekuwa na fadhaa. Unahofia kushikwa na nyingine. Hiyo ni kweli. Iwapo hiyo ni kweli, inua mkono wako, unapofuta machozi yako kutoka machoni mwako. Usiogope, na hutakuwa nayo.

¹⁰⁶ Mama anayeketi karibu nawe hapo, una pumu, ugonjwa wa mkamba. Acha kuvuta sigara, utakuacha.

¹⁰⁷ Mwamini Mungu. Amini kwa moyo wako wote. Kama unaweza kuamini, mambo yote yanawezekana!

¹⁰⁸ Huyu hapa mama ameketi moja kwa moja nyuma ya mama huyu hapa. Nina hakika wewe ni... Mama huyu, hebu kidogo, jina lake ni Bibi Evans. Anatoka Kentucky, Louisville. Hiyo ni kweli. Sikujui mimi. Unajua hiyo ni kweli. Una ugonjwa wa moyo, una matatizo ya masikio yako. Hiyo ni kweli. Kama hiyo ni kweli, inua mkono wako. Rudi Louisville, Yesu Kristo anakuponya.

¹⁰⁹ Ninaitolea imani yako changamoto, katika Jina la Yesu Kristo, kuliadini. Mtu yeyote humu ndani, amini kwa moyo wako wote! Huko nyuma kabisa, unayesimama nyuma kabisa, wewe amini. Sio lazima uwe mahali fulani maalum. Huku upande *huu*, amini! Ni wangapi huko nyuma wanaohitaji uponyaji? Inueni mikono yenu, na kusema, “Ninaamini, Bwana.” Iweni na imani!

¹¹⁰ Ninamwona mtu ambaye anaomba kwa uaminifu, ameketi moja kwa moja upande *huu* hapa, katika ono, amesimama hapo, yeye ni mhubiri, amesimama karibu na mimbara, naye anahubiri apate ongezeko... anaombea ongezeko katika huduma yake. Sijawahi kumuona awali maishani mwangu. Lakini hilo ndilo unaloombea, ndugu. Utalipata sasa. Mwamini Bwana Yesu!

¹¹¹ Kuna mtu ameketi nyuma yake hapo, ambaye ana kasoro fulani kwenye mkono wake, mafundo mkononi mwake. Yeye pia... Kama utaamini, bwana, unaweza kupokea uponyaji wako. Amina.

¹¹² *Huku* nje tu mwishoni mwa safu hii hapa, ya pili ndani, maskini mama aliyeinamisha kichwa chake, moja kwa moja kuelekea nyuma, ameketi hapo akiomba, ana ugonjwa wa kibofu nyongo. Jambo ndilo hilo, mama, uliinua mkono wako, nami ninajua wewe—wewe ndiwe uliyekuwa unaomba. Ulipokea uponyaji wako wakati uo huo.

¹¹³ Vipi kuhusu hilo, unaamini kwamba Yesu alifufuka katika wafu? Yuko hapa sasa? Unamwamini? Basi kama mtaniamini, kama nimewaambia Ukweli wa Biblia, naye Mungu amegeuka na kuthibitisha kuwa nimewaambia Kweli, hiyo ina maana kwamba, kikamilifu kwamba, Bwana Yesu yuko hapa. Je, hiyo ni kweli?

¹¹⁴ Basi ninyi fanyeni hivi, fanyeni hivi, msitilie shaka, weka mikono yako juu ya mtu anayeketi karibu nawe. Nitaomba kutoka papa hapa, na kundi lote lenu litaponywa sasa hivi kama mtaamini. Mtaamini? Wekeaneni mikono, basi. Nyote mnaoamini kuwa mtaponywa sasa, semeni, “Amina.” [Kusanyiko linasema, “Amina.”—Mh.] Sasa wewe... Nitasema ombi hili. Ninyi ombeni, ombeni nyuma yangu:

¹¹⁵ Ee Bwana, Muumba wa Mbingu na nchi, Mwanzilishi wa Uzima wa milele, Mpaji wa kila karama njema, nina haja, Bwana, na nguvu Zako za uponyaji. Nami naomba ya kwamba utanipa imani kuukubali. Hiyo ni ahadi Yako. Ninaamini ya kwamba Wewe ndiwe Yesu yeye yule aliyetembea kwenye pwani za Galilaya, aliyeteswa chini ya Pontio Pilato, akafa, akafufuka, akapaa Juu, akawapa wanadamu vipawa tena, kwa njia ya Roho Mtakatifu. Ninaamini Roho Mtakatifu yuko hapa akiendelea na kazi ile ile uliyofanya ulipokuwa hapa. Ninaikumbatia ahadi hiyo. Ninakubali uponyaji wangu. Ninaahidi kukuishia Wewe na kutii Amri Zako, kutembea katika Nuru. Na sasa ninaamini, kwa sababu nimefanya maungamo haya, ya kwamba nimeponywa kwa kupigwa Kwako.

¹¹⁶ Ketini kimya kabisa. Sasa wazia tu, hayo ni maungamo yako, Mungu anaingia ndani yako sasa hivi. Mvuteni ndani Roho Mtakatifu, kwa imani, “Ninaamini kwamba ugonjwa wangu unaponywa. Ninaamini kuwa ugonjwa wangu wote umeondolewa.” Sasa hivi mko Mbele za Mungu. Hivi hamwezi kumhisi Roho huyo? Fungueni mioyo yenu, i—imani yenu. Roho Mtakatifu anawaponya watu sasa hivi; msichana mdogo anayeketi tu hapa, mwingine mkono wangu wa kulia. Jukwaa zima linaonekana kuangazwa na Nguvu za Kristo aliyefufuka. Yeye yuko juu ya hili kusanyiko. Yuko ndani ya watu. Sasa, hayo yalikuwa maombi yako.

¹¹⁷ Sasa nitaomba na kumwagiza ibilisi wa mashaka awaondokee.

¹¹⁸ Ee Bwana Mungu, Muumba wa Mbingu na nchi, uyasikie maombi yangu, Bwana; upesi, wakati Roho Mtakatifu yuko

hapa, kabla watu hawajaangamia.

¹¹⁹ Ninamhukumu ibilisi. Yesu Kristo alikunyang'anya ushindi, alipata ushindi pale Kalvari; alishinda mauti, ibilisi, kuzimu, na kaburi, na kufufuka tena siku ya tatu, naye yu hai hata milele. Toka hapa, Shetani, wewe ni kiumbe kilichoshindwa. Waache watu hawa, na wapate kuponywa, katika Jina la Bwana Yesu Kristo.

¹²⁰ Wote mnaoukubali uponyaji wenu, simameni kwa miguu yenu sasa hivi. Katika Jina la Yesu Kristo, simameni! Amina. Mwinulieni mikono yenu, mkamsifu. Watu pekee ninaowaona ambao hawajasimama, kuna mwanamume anayeketi hapa kwenye kiti cha magurudumu, Gane Heelie. Najua ugonjwa wake, ana ugonjwa wa polio.

¹²¹ Inaonekana kama kiti cha magurudumu *hapa* nyuma. Hebu tuone. Kuna mgonjwa, mwanamke mwenye mguu mmoja. Je, hiyo ni kweli? Je, unaniamini mimi kuwa ni nabii wa Mungu? Hatufahamiani. Siwezi kukuponya. Lakini unaamini Mungu anaweza kuniambia shida yako ni nini? [Dada huyo anasema, "Ndiyo."—Mh.] Ikiwa ingeweza, ingekusaidia? Una ugonjwa wa kisukari. Hiyo ni kweli. Sasa amini, na uende nyumbani uwe mzima, kwenye kiti cha magurudumu. Hayo tu ndiyo unayopaswa kufanya, ni kumwamini Bwana Yesu Kristo, na upone!

¹²² Inueni mikono yenu sasa, na—na kusema, "Asante, Bwana, kwa kuniponya. Asante, Bwana, kwa kuniponya. Ninakusifu, Bwana, kwa kuniponya. Mungu ni mwema! Mungu ni mkuu! Mungu ni wa thamani! Mungu ni halisi! Mungu yuko hapa! Roho Mtakatifu yuko hapa. Nguvu za Mungu ziko hapa. Na sasa ninaamini kwa yote yaliyo ndani yangu, ya kwamba Yesu Kristo, Mwana wa Mungu, ananiponya. Amina."

¹²³ Ikiwa kuna yeyote hapa ambaye amehukumiwa dhambi, na unajua kwamba dhambi zako haziko chini ya Damu, na sasa hivi katika Uwepo wa Mungu, Yeye anayejua mawazo yako, naye Roho Mtakatifu ananiambia hivi, ungependa kumkubali kama Mwokozi wako binafsi, ungetaka kukumbukwa katika maombi? Inueni mikono yenu, wote walioko hapa ndani. Mungu akubariki, na wewe, na wewe, na wewe, na wewe. Hiyo ni sawa. Huko nyuma, wewe, na hapa. Hakika. Huku nyuma, Mungu akubariki, mwanangu. Mungu akubariki hapo. Na Mungu akubariki. Hiyo ni kweli.

¹²⁴ Mnaona, Roho Mtakatifu hakosei kamwe. Roho Mtakatifu anaposema... Nilikuwa nikijiandaa kumrudishia Ndugu Neville ibada, kwa maana uponyaji umekwishia, lakini Kitu fulani kikasema, "Wanahitaji uponyaji wa nafsi." Ikiwa unataka kumpokea Yesu kama Mwokozi wako binafsi, inamisha kichwa chako kwa muda kidogo. Na tuombe.

¹²⁵ Ndugu Neville, nimepwelewa sana na sauti, wewe omba ombi hili, sivyo. Vema.

¹²⁶ [Ndugu Neville anaomba, “Baba wa Mbinguni, katika Jina la Bwana Yesu Kristo, Yeye aliyetembea kwa utukufu hapa kati yetu usiku wa leo, wakati hawa wanaoinamisha vichwa vyao kwa imani usiku wa leo, wakiadini ya kwamba Wewe unaweza kuwakomboa, nafsi na mwili pia, waokoe wale wanaoamini sasa katika imani yenye toba. Mungu mpendwa, naomba usiku huu uwe usiku tofauti kwao. Wape shauku sasa, Ee Mungu. Na uwape sasa, Ee Bwana Yesu, ujuzi huo unaotamanika sana wa dhambi zilizosamehewa. Okoa kila mmoja, Ee Mungu, walioinamisha vichwa vyao huko nje, walioonyesha shauku ya kuombewa. Pia wajalie, tangu wakati huu na kuendelea, jalia wakusudie moyoni mwao kuishi kwa ajili Yake aliyewafia. Katika Jina la Yesu na kwa ajili ya Yesu tunaomba. Amina, na amina. Bwana asifiwe!”—Mh.] 

59-0329^E Ishara Ya Masihi
Branham Tabernacle
Jeffersonville, Indiana Marekani

SWAHILI

©2022 VGR, ALL RIGHTS RESERVED

VOICE OF GOD RECORDINGS
P.O. Box 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.
www.branham.org

Ilani ya haki ya kunakili

Haki zote zimehifadhiwa. Kitabu hiki kinaweza kuchapishwa kwa matbaa ya nyumbani kwa matumizi ya kibinafsi ama kusambaza, bila malipo, kama chombo cha kuitangazia Injili ya Yesu Kristo. Kitabu hiki hakiwezi kikauzwa, kunakiliwa kwa wingi, kuwekwa kwenye mtandao, kuhifadhiwa kikatolewe tena, kufasiriwa katika lugha zingine ama kutumiwa kuomba fedha bila idhini halisi iliyoandikwa moja kwa moja kutoka Voice Of God Recordings®.

Kwa habari zaidi ama kwa vifaa zaidi, tafadhali wasiliana na:

VOICE OF GOD RECORDINGS

P.O. BOX 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.

www.branham.org